HALMASHAURI YA WILAYA MASASI

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: **2510031,**
Fax: **2510045.**
E-mail: **ded@.masasidc.go.tz**
Website: **www.masasidc.go.tz**

S.L.P. 60,
Masasi,
Mtwara**,**

Kumb. Na. MDC/R.30/……. Tarehe: 23 Julai, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti,
Waheshimiwa Wajumbe,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Wilaya,
MASASI.

YAH: TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA JULAI 2017 – JUNI, 2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kumaliza mwaka wa fedha 2017/2018 salama. Pia ni jambo la kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuitumikia Halmashauri yetu kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya awamu ya tano.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana Wah. Madiwani wote, viongozi wote katika ngazi ya Wilaya hasa Mkuu wa Wilaya, Kamati ya Ulinzi na Usalama (W), Wakuu wa Idara, Watendaji wote wa Kata na Vijiji na kwa namna ya pekee wenyeviti wote wa vijiji na vitongoji kwa kutekeleza majukumu yao vizuri na kwa ufanisi. Kwa namna ya pekee nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wah. Wabunge wote kwa ushirikiano wao mkubwa na ushauri kila ulipohitajika.

Lakini pia niwashukuru viongozi wote wa vyama vya Siasa, wadau wote wa maendeleo kwa ushirikiano mkubwa mlioutoa ndani ya Halmashauri katika kipindi cha mwaka mzima. Mwisho lakini si kwa umuhimu niwashukuru sana watumishi wote ambao kwa ushirikiano wao na utendaji wao tumeweza kufanya na kutekeleza mipango mingi.

Mhe. Mwenyekiti naomba nitoe taarifa ya utendaji kazi wa Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2017 hadi Juni, 2018.

Katika kipindi tajwa, Halmashauri iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufuata sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizowekwa na Serikali.
Aidha, majukumu yote yalitekelezwa kwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kufuata Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/17.

2. Ilani ya Chama Tawala 2015-2020.
3. Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021.
4. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.
5. Kushughulikia mambo yote ya dharura yaliyohitaji utekelezaji wa haraka.
6. Kutekeleza maagizo yote yaliyotoka ngazi za juu, yaliyoagizwa na Kamati mbalimbali pamoja na yale yaliyotolewa na Baraza lako tukufu.

A. MAPATO

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi **27,503,742,000.00,** kati ya fedha hizo; shilingi **2,484,576,000.00** ni mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri, **19,264,953,000.00** kwa ajili ya mishahara (Serikali kuu), **1,043,086,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo (Serikali kuu) na **4,711,127,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Serikali kuu). Hadi kufikia Juni 30, 2018 jumla ya shilingi **34,849,772,550.82** zilikusanywa sawa na asilimia **126.71** ya bajeti yote ya mwaka wa fedha 2017/18 kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na.1: Muhtasari wa Mapato kuishia Juni 30. 2018

ENEO	MAKISIO 2017/2018	MAPATO JULAI 2017 – JUNI,2018	ASILI MIA
Mapato ya Ndani (Matumizi mengineyo)	945,386,400.00	1,438,661,400.90	152.18
Mapato ya Ndani (Miradi ya Maendeleo)	1,539,189,600.00	757,837,659.20	49.24
Jumla ya Mapato ya Ndani	**2,484,576,000.00**	**2,196,499,060.10**	**88.41**
Ruzuku ya Fidia (GPG)	184,289,000.00	148,718,000.00	80.70
Mishahara (PE)	19,264,953,000.00	17,265,668,333.79	89.62
Matumizi Mengineyo (Other Charges)	858,797,000.00	713,013,800.00	83.02
Jumla Ndogo	**20,308,039,000.00**	**18,127,400,133.79**	**89.26**
Miradi ya Maendeleo			
LG – CDG	1,400,444,000.00	400,000,000.00	28.56
Ofisi za Halmashauri	600,000,000.00	600,000,000.00	100
Mfuko wa Jimbo	76,975,000.00	76,975,000.00	100
Elimu bila malipo shule za Msingi	730,353,000.00	809,279,586.00	110.8
Elimu bila malipo shule za Sekondari	945,128,000.00	1,184,824,244.29	125.36
Mfuko wa Afya wa Pamoja	532,622,000.00	494,137,700.00	92.77
Miradi ya Maji vijijini	342,931,000.00	77,872,471.05	22.71
UNICEF	82,674,000.00	121,260,890.00	146.67
Jumla Ndogo	**4,711,127,000.00**	**3,764,349,891.34**	**79.90**
JUMLA KUU- BAJETI 2017/2018	**27,503,742,000.00**	**24,088,249,085.23**	**87.58**
FEDHA ZILIZOPOKELEWA NJE YA BAJETI			
Boresha Afya (DELOITE)	0.00	25,285,000.00	0.00
TASAF	0.00		0.00

		4,191,068,271.59	
Mfuko wa Wanawake na Vijana	0.00	16,000,000.00	0.00
Miradi wa Maji	0.00	3,509,788,036.05	0.00
Magonjwa yasiyopewa kipaumbele	0.00	89,983,031.84	0.00
UNICEF	0.00	5,646,400.00	0.00
Ujenzi wa Kituo cha Afya-Nagaga	0.00	400,000,000.00	0.00
Mishahara ya watumishi wapya Idara ya Afya	0.00	14,224,000.00	0.00
Ujenzi wa miundombinu shule ya Sekondari Ndwika na Chidya (EP4R)	0.00	800,000,000.00	0.00
Ujenzi wa Miundombinu shule ya Msingi, Chidya,Chiwata na Nairombo (EP4R)	0.00	239,800,000.00	0.00
Mfuko wa Amana	0.00	1,469,728,726.11	0.00
JUMLA NDOGO	**0.00**	**10,761,523,465.59**	
JUMLA KUU- MAPATO YOTE	**27,503,742,000.00**	**34,849,772,550.82**	**126.71**

Mhe. Mwenyekiti mapato haya yameonekana kutofautiana sana na makadirio kwa sababu ya kupokelewa kwa kiasi cha Shilingi **9,291,794,739.48** ambazo zilikua hazipo katika bajeti ya mwaka 2017/18. Pia Serikali kupitia sera ya "Elimu bila Malipo" na mradi wa UNICEF imeleta fedha zaidi ya zile zilizokuwepo kwenye mpango na bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2017/18

B. MATUMIZI:

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri ilikadiria kutumia jumla ya shilingi **27,503,742,000.00** kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matumizi yaliyofanyika hadi kufikia Juni 30, 2018 ni shilingi **33,956,430,766.35** ambayo ni sawa na asilimia **123.46** ya bajeti yote ya mwaka wa fedha 2017/18 kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na.2: Muhtasari wa Matumizi kuishia Juni 30, 2018

ENEO	MAKISIO 2017/2018	JUMLA YA MATUMIZI JULAI 2017 – JUNI 2018	ASILIMIA
Mapato ya Ndani (Matumizi Mengineyo)	945,386,400.00	1,488,066,945.12	157.40
Mapato ya Ndani (Miradi ya maendeleo)	1,539,189,600.00	702,952,236.64	45.67
Jumla ya Mapato ya Ndani	**2,484,576,000.00**	**2,191,019,181.76**	**88.18**
Ruzuku ya Fidia (GPG)	184,289,000.00	148,566,853.79	80.62
Mishahara (PE)	19,264,953,000.00	17,265,668,333.79	89.62
Matumizi Mengineyo (Other Charges)	858,797,000.00	702,876,424.95	81.63

Jumla Ndogo	**20,370,043,000.00**	**18,117,111,612.53**	**88.94**
Miradi ya Maendeleo			
LG - CDG	1,400,444,000.00	0.00	0.00
Ofisi za Halmashauri	600,000,000.00	599,185,010.62	99.86
Mfuko wa Jimbo	76,975,000.00	63,657,077.00	82.70
Elimu bila malipo shule za Msingi	730,353,000.00	809,279,586.00	110.81
Elimu bila malipo shule za Sekondari	945,128,000.00	1,184,824,244.29	125.36
Mfuko wa Afya wa Pamoja	532,622,000.00	493,687,390.65	92.69
Miradi ya Maji vijijini	342,931,000.00	77,868,677.83	22.71
UNICEF	82,674,000.00	121,260,890.00	146.67
Jumla miradi ya Maendeleo	**4,711,127,000.00**	**3,349,762,876.39**	71.10
JUMLA BAJETI 2017/2018	**27,503,742,000.00**	**23,657,893,670.68**	**86.02**
MATUMZI NJE YA BAJETI			
Boresha Afya (DELOITE)	0.00	25,148,480.00	0.00
TASAF	0.00	4,191,068,271.59	0.00
Mfuko wa Wanawake na Vijana	0.00	110,545,000.00	0.00
Miradi wa Maji	0.00	3,509,788,036.05	0.00
Magonjwa yasiyopewa kipaumbele	0.00	89,979,805.56	0.00
UNICEF	0.00	0.00	0.00
Ujenzi wa Kituo cha Afya - Nagaga	0.00	400,000,000.00	0.00
Mishahara ya watumishi wapya Idara ya Afya	0.00	7,751,200.00	0.00
Ujenzi wa miundombinu shule ya Sekondari Ndwika na Chidya (EP4R)	0.00	643,870,113.00	0.00
Ujenzi wa Miundombinu shule ya Msingi, Chidya,Chiwata na Nairombo (EP4R)	0.00	182,535,300.00	0.00
Mfuko wa Amana	0.00	1,137,850,889.47	0.00
Jumla Ndogo		**10,298,537,095.67**	0.00
JUMLA KUU MATUMIZI	**27,503,742,000.00**	**33,956,430,766.35**	**123.46**

Mhe. Mwenyekiti matumizi hayo hayalingani na makisio ya mapato kwa sababu zifuatazo:

1. Jumla ya shilingi **9,152,935,006.20** zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Sekta ya Maji, TASAF, Elimu, Afya na Maendeleo ya Jamii fedha ambazo zilikua hazipo katika mpango na bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2017/18.

2. Halmashauri imetumia fedha zaidi ya zile zilizopo kwenye mpango na bajeti yake hii imetokana na Serikali kupitia sera ya "Elimu bila Malipo" na mradi wa UNICEF kuleta fedha zaidi ya zile zilizokuwepo kwenye mpango na bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2017/18 kama inavyoonekana katika majedwali hapo juu.

C. SALIO KWENYE AKAUNTI ZA HALMASHAURI KWA MWAKA 2017/18

Hadi kufikia Juni 30, 2018 Halmashauri ilikuwa na salio la shilingi **869,340,757.82** katika akaunti zote nane. Sababu kuu ya kuwepo kwa salio hilo ni:

- Serikali Kuu kuchelewa kuleta fedha za miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha shilingi **400,000,000.00** kimepokelewa mwishoni mwa robo ya nne ya mwaka wa fedha 2017/18 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Chiungutwa.
- Uwepo wa fedha za wakandarasi kwa kipindi cha matazamio na wanaoendelea na kazi hususani za miradi ya maji na ujenzi wa Ukumbi na Ofisi za Halmashauri (Retention money) katika akaunti ya Amana.

D: MASUALA YA DHARURA:

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri ilipokea wageni mbalimbali kutoka Serikali, Wageni hao ni:-

1. Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa – Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
2. Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe - Waziri wa Maji
3. Mhe. George Joseph Kakunda - Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tamisemi Elimu
4. Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa - Naibu Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji na Ushiriki
5. Mhe. Dkt. Zainabu Chaula- Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI

E. MATUMIZI YA FEDHA KWA SHUGHULI ZA MAENDELEO

i) MAPATO YA NDANI (OWN SOURCE)

Mhe. Mwenyekiti kwa mwaka wa fedha 2017/18 kiasi cha shilingi **291,617,436.08** kimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo; Shilingi **93,693,192.23** zimetumika kununua gari la kufuatilia mapato**, 25,379,243.85** zimetumika kujenga miundombinu katika shule za msingi, **122,545,000.00** zimetumika kutoa mikopo kwa vikundi **55** vya wanawake na vijana pamoja na **50,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi Ndanda ambapo maandalizi ya ujenzi yanaendelea.

ii) MATUMIZI YA MFUKO WA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti katika mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri ilihuwisha Mfuko wa Elimu kwa lengo kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya Elimu na ilijiwekea lengo la kukusanya shilingi **570,000,000.00** kutoka kwa wadau mbalimbali, hadi kufikia Juni 30, 2018 kiasi cha shilingi **500,800,000.00 (87.86)** kilikusanya na kilitutumika katika ujenzi wa vyumba **24** vya madarasa, matundu **208** ya vyoo, nyumba **2** za Walimu, ukarabati wa vyumba **11** vya madarasa ujenzi wa vyumba **24** vya madarasa, matundu **208** ya vyoo, nyumba **2** za Walimu, ukarabati wa vyumba **11** vya madarasa na kuajili Walimu **2** wa muda mfupi

iii) RUZUKU YA MAENDELEO (LGCDG)

Mhe. Mwenyekiti kiasi cha shilingi **400,000,000.00** kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Chiungutwa, taratibu za kuanza ujenzi huo zinaendelea.

iv) UJENZI WA UKUMBI WA MIKUTANO NA OFISI ZA HALMASHAURI

Mhe. Mwenyekiti jumla ya shilingi **631,500,000.00** zimetumika kuendeleza ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano na Ofisi za Halmashauri ambapo ujenzi wa sakafu (*first floor*) na Ukumbi upo katika hatua ya ukamilishaji.

v) UJENZI NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU SHULE ZA SEKONDARI

Mhe. Mwenyekiti shule ya Sekondari Ndwika ilipokea shilingi **400,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa mabweni **2**, vyumba **7** vya madarasa, Jengo la Utawala na jengo la Maabara ya Jiografia ambopo jumla ya shilingi **361,463,451.11** zilitumika. Kiasi cha shilingi **38,536,548.89** kilichobakia kinaendelea kujenga mabweni **2** viporo.

Shule ya Sekondari Chidya ilipokea shilingi **400,000,000.00** kwa ajiri ya kukarabati madarasa **8**, mabweni **2**, jengo la utawala, jiko, Maktaba, Karakana, jengo la Idara mbalimbali za masomo, mfumo wa maji pamoja na ujenzi wa nyumba **1** ya Mwalimu ambapo jumla ya shilingi **256,204,913.00** zilitumika. Kiasi cha shilingi **143,795,087.00** kilichobaki kilitumika katika umaliziaji wa mabweni **2** na ununuzi wa samani za mabweni hayo pamoja na kujenga vyumba vipya **3** vya madarasa.

vi) UJENZI WA MIUNDOMBINU KATIKA SHULE ZA MSINGI

Mhe.Mwenyekiti jumla ya shilingi **182,535,300.00** zimetumika kujenga vyumba **11** vya madarasa na matundu **18** ya vyoo katika shule ya Msingi Chidya, Chiwata na Nairombo.

vii) UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA.

(a) Mhe. Mwenyekiti jumla ya shilingi **400,000,000.00** zimetumika kujenga Maabara, Jengo la upasuaji, Wodi ya wazazi, Jengo la kuhifadhia maiti na nyumba ya Mganga katika kituo cha Afya Nagaga.

(b) Halmashauri iliendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Mnavira ambapo jumla ya shilingi **25,000,000.00** zimetumika.

(c) Halmashauri ilitoa kiasi cha shilingi **11,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati ya Chiwata ambapo kazi ya ukamilishaji inaendelea.

viii) MIFUKO YA MAJIMBO.

Mhe. Mwenyekiti jumla ya shilingi **63,657,077.00** zimetumika kusaidia utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo katika majimbo ya Ndanda na Lulindi**.**

ix) MRADI WA KUNUSURU KAYA MASIKINI (TASAF)

Mhe. Mwenyekiti jumla ya shilingi **4,191,068,271.59** zimetumika kusaidia kaya masikini na kufanya malipo katika ajira za muda kwa miradi iliyoibuliwa na kutekelezwa. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:- Mradi wa visima **30** vya kuchimbwa kwa mikono, miradi **61** ya upandaji miti, miradi **4** ya uboreshaji wa mabwawa na mradi **1** wa uboreshaji wa miundombinu ya maji imetekelezwa.

x) MRADI WA MAJI VIJIJINI (NWSSP)

Mhe. Mwenyekiti jumla ya shilingi **3,509,788,036.05** zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maji vijijini. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa maji Mkululu - Mpopo, Mkululu - Majembe, Mpindimbi – Shaurimoyo, Chipingo – Manyuli – Mkaliwata, Chiwambo – Nagaga, Nagaga – Mpeta, Nagaga – Mirewe, Mwena – Liloya, Makong'onda - Livango na Chiungutwa,

xi) MRADI WA KUBORESHA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI

Mhe. Mwenyekiti jumla ya shilingi **1,994,103,830.29** zimetumika kuboresha elimu katika shule za Msingi na Sekondari ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia, chakula kwa shule za bweni na Fedha kwa ajili ya madaraka kwa Waratibu Elimu kata na Walimu Wakuu.

xii) MRADI WA UNICEF

Mhe. Mwenyekiti jumla ya shilingi **121,260,890.00** zimetumika katika zoezi la usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa. Watoto **30,970** wenye umri chini ya miaka mitano ikiwa sawa na asimia **87** ya lengo la kuandikisha watoto **35,720** wamesajiliwa.

xiii) FEDHA ZA P4R MOTISHA

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri ilipokea kiasi cha shilingi **115,272,993.23** kutoka Wizara ikiwa ni motisha ya upangaji wa ikama ya Walimu kwa shule za Msingi na Sekondari. Fedha hizo zilitumika katika zoezi la ukusanyaji wa takwimu za elimu na ufuatiliaji wa taaluma shuleni, Upangaji wa Ikama ya Walimu shule za msingi, mpango wa umaliziaji wa vyumba **2** vya madarasa shule ya sekondari Chiwale, ujenzi wa vyumba **3** vya madarasa katika shule ya msingi Mbemba, Nakalala na Lusonje pamoja na ukamilishaji wa maabara **4** katika shule ya Sekondari Chiungutwa, Mwena, Chiwata na Mkalapa. Fedha zimepelekwa tayari kwa mchakato wa kutekeleza shughuli hizo.

F. MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/18 Jumla Kaya **20,436** zenye wanachama **102,426** walijiunga na mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) sawa na asilimia **29.67** ya kaya **68,887** na asilimia **38.69** ya wananchi **264,765** waliopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Uhamasishaji unaendelea katika ngazi ya vijiji ili kuhakikisha wananchi wote wanajiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).

G. USHIRIKIANO WETU WA MASASI NA ENZKREIS – UJERUMANI

Mhe. Mwenyekiti, ushirikiano wetu na Enzkreis umezidi kuimarika kijamii na kiutendaji. Mwaka 2016/17, Halmashauri kwa kushirikiana na Enzkreis iliingia Mkataba na kampuni ya **Ensol Tanzania Limited** wa kufunga mfumo wa umeme jua (Solar System) kwenye zahanati **27** (Zahanati **22** za Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na **5** za Halmashauri ya Mji Masasi), hadi kufikia mwezi Juni, 2018 kazi imekamilika kwa asilimia **95** na jumla ya shilingi **496,462,179.00** kati ya shilingi **599,996,468.00** ya Mkataba zimetumika na shilingi **95,567,661.00** zimelipwa kwa Mtaalam Mshauri – **TAREA** na gharama za kuwasafirisha wageni kutoka Ujerumani wakiwa nchini Tanzania.

H. WATUMISHI:

Mhe. Mwenyekiti, Hadi kufikia Juni 30, 2018 Halmashauri ilikuwa na jumla ya watumishi **1,972** kati ya **3,531** wanaohitajika, hivyo kufanya upungufu wa watumishi **1,559.**

- Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Halmashauri imefanikiwa kuajiri watumishi **101**, kati ya hao, Walimu wa Sekondari **5**, Walimu wa Msingi **2**, Idara ya Afya Watumishi **8** na Idara ya Utawala Watumishi **86** (Watendaji wa Vijiji **81**, Watendaji wa Kata **3**, Afisa Ugavi **1** na Afisa Nyuki **1**).
- Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Watumishi **68** walihama kutoka Halmashauri yetu, Watumishi **30** wamehamia, Watumishi **44** walistaafu, Watumishi **09** walifariki dunia na Mtumishi 1 aliacha kazi.

- Watendaji wa Vijiji wenye elimu ya darasa la saba **78** waliondolewa katika Utumishi wa Umma mwezi Julai 2017. Watumishi hao walirejeshwa kazini mwezi Aprili, 2018 ili waendelee na kazi hadi watakapostafu. Jumla ya Watendaji wa Vijiji **74** walirejeshwa katika mfumo wa mishahara. Watumishi **4** hawajarejeshwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo; Watumishi **2** walistaafu, **1** alighushi vyeti na **1** alifariki.

  Kutokana na kurejeshwa kazini kwa Watumishi hao, Vijiji vyote katika Halmashauri yetu vimepata Watendaji wa vijiji.

- Katika kipindi cha mwaka 2017/18 Halmashauri ilipeleka Watumishi **29** katika mafunzo ya muda mrefu. Pia Watumishi **42** walikua wanaendelea na mafunzo kama hayo katika vyuo mbalimbali, hivyo jumla ya Watumishi **71** walikuwa masomoni. Watumishi 55

walipata mafunzo ya muda mfupi ya kujengewa uwezo na Watumishi **128** wa ajira mpya walipata mafunzo elekezi.

I. UPIMAJI ARDHI MAENEO YA VIJIJINI NA MIJI MIDOGO

Mhe. Mwenyekiti upimaji wa maeneo ya vijijini unaendelea, mpaka Juni, 2018 taasisi za serikali **24** zimepimwa na mashamba ya wananchi **212** yamepimwa. Kwa maeneo ya miji midogo jumla ya michoro **2** ya Mipango Miji (TP) katika maeneo ya Nagaga na Lukuledi imeandaliwa. Katika michoro hii Nagaga kuna jumla ya viwanja **222** vya matumizi mbalimbali ikiwemo ekali **18** zimetengwa kwa ajili ya viwanda vidogo. Katika eneo la Lukuledi jumla ya viwanja **596** vimeandaliwa kwa matumizi mbalimbali ikiwemo ekali **20** zilizotengwa kwa ajili ya viwanda vya kati. Taratibu za upimaji wa maeneo haya zinaendelea.

J. HUDUMA ZA AFYA

a. Upatikanaji wa dawa

Mhe. Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba umekuwa wa kuridhisha kutokana na ukweli kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya dawa, vitendanishi na vifaa tiba ni kwa asilimia **100** kwa fedha zinazotoka Wizara ya Afya kwenda Bohari ya Dawa (receipt in kind), Pesa za Mfuko wa CHF, Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) na Mfuko wa Afya wa pamoja (HSBF). Mtiririko wa taarifa kutoka vituo vya kutolea huduma za afya kwenda Wilaya, LMU na MSD ni za wakati katika robo zote nne kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

b. Miradi msonge (Vertical Programs)

Mhe.Mwenyekiti, Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18 imeweza kutekeleza miradi mbalimbali kama ifuatavyo:

- Ugawaji wa dawa za Malaria (ARU).
- Ugawaji wa dawa kwa watu wanaoishi na VVU.
- Ugawaji wa dawa za uzazi wa mpango.

K. HUDUMA ZA KIJAMII

a. Huduma kwa makundi maalum

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri imeweza kuwapatia vifaa watu **83** wenye ulemavu mbalimbali. Miongoni mwao wapo wenye ulemavu wa ngozi, viungo na wasioona. Vifaa vilivyotolewa ni mguu 1 wa bandia uliogharimu shilingi **625,000.00**, Baiskeli za kusukuma (*wheel chair*) 2 zilizogharimu shilingi **1,100,000.00**, mafuta ya ngozi chupa **30** yaliyogharimu shilingi **750,000.00**, kofia za kujikinga na jua **35** zilizogharimu shilingi **350,000.00**, Magongo **5** yakutembelea yaliyogharimu shilingi **475,000.00** na fimbo nyeupe **10** ambazo zimegharimu shilingi **250,000.00.** Aidha katika kuimarisha huduma za kijamii Halmashauri imeweza kuwasaidia watoto **150** walio katika mazingira hatarishi (*Most Vulnerable Children*) kwa kuwapatia sare za shule na vifaa vya darasani.

b. Uwezeshaji wa Vikundi vya Wanawake na Vijana

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi **299,264,000.00** katika vikundi **100** vya Wanawake na Vijana. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo; Halmashauri imechangia kiasi cha shilingi **122,545,000.00** kutoka mapato yake ya ndani kwa vikundi **55** vya Wanawake na Vijana, Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii shilingi **20,000,000.00** ambazo zimetolewa kwa vikundi **7** vya Wanawake na shilingi **156,719,000.00** fedha za marejesho ambazo zimetolewa kwa vikundi **38** vya Wanawake na Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Baraza la uwezeshaji Wananchi kiuchumi imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi **63,500,000** kwa vikundi **12** vya **VICOBA**.

L. UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauria ya Wilaya inasimamia utekelezaji wa Sheria, Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya mazingira na udhibiti wa taka ngumu. Kwa mwaka 2017/18 jumla ya miti **852,232** imepandwa ambayo ni sawa na asilimia **56** ya utekelezaji wa lengo la mwaka. Pia Halmashauri imefanya ukaguzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika Viwanda, Migodi, na vituo vya kuuza mafuta.

M. USIMAMIZI WA KESI ZA HALMASHAURI

Mhe. Mwenyekiti kwa kipindi cha mwaka 2017/18 Halmashauri iliweza kusimamia jumla ya kesi **5** ambapo kati ya kesi hizo Halmashauri ilishinda kesi **1** na ilishindwa kesi **1**.

Katika kesi hizo **5,** kesi **1** iliisha kwa makubaliano na mdai (Tecno Classic) kwa kumlipa kiasi cha shilingi **15,024,155.00** ambazo mdai amesharipwa zote kwa makubaliano nje ya mahakama, kiasi cha shilingi **10,000,000.00** kimelipwa kwa mdai (Ally Mfaume) kwa shauri ambalo liliisha tangu mwaka 2014, pia katika mwaka 2018/19 kiasi cha shilingi **5,000,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kumlipa mdai (Juma Jabu).

N. USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA KILIMO NA MIFUGO

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri imeendelea kusimamia na kuendeleza kilimo katika Kata zake zote **34**, kwa mwaka wa fedha 2017/18 miongoni mwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na:-

i) Ugawaji wa miche kwa kata zote 34. Jumla ya miche **645,280** imesambazwa
ii) Ukusanyaji wa taarifa za wakulima wa korosho na wakulima wa mazao wengine ili kuwa na takwimu za uhakika
iii) Uhamasishaji na ufufuaji wa kilimo cha Alizeti katika Kata za Namatutwe, Msikisi, Namajani, Chigugu, Chiungutwa, Ndanda, Namalenga na Nangoo kwa kushirikiana na Agha Khan foundation
iv) Kushiriki maonesho ya wakulima nane nane kitaifa Ngongo – Lindi, ambapo halmashauri iliibuka mshindi wa kwanza kwenye kundi la serikali za mitaa.
v) Kushiriki mafunzo juu ya uzalishaji wa mbegu za muhogo kibiashara kwa Waheshimiwa madiwani wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi

vi) Ukarabati wa milango ya banio katika skimu za umwagiliaji za Ndanda na Mkungu. Jumla ya shilingi **6,960,000.00** zimetumika.

vii) Ukarabati wa jengo la kiwanda cha kusindika muhogo Mpanyani na ufungaji wa mashine ya kusaga. Jumla ya shilingi **2,560,560.00** zimetumika

viii) Ukarabati wa mashine za kusindika Alizeti Mpanyani na Mbuyuni kwa kushirikiana na Agha Khan foundation. Kwa sasa mashine zote zinakamua mafuta. Jumla ya shilingi **2,800,000.00** zimetumika

ix) Kusimamia ununuzi wa korosho kwa msimu wa 2017/2018, ambapo Jumla ya kilo **28,773,714** zilikusanywa. Hadi Juni 30, 2018 bado baadhi ya wakulima wanadai fedha zao.

x) Kusimamia mikutano mikuu ya mwaka 2017/2018 ya vyama vya msingi, ambapo jumla ya mikutano **42** ilifanyika.

xi) Kupiga chapa ya moto mifugo iliyopo katika Halmashauri yetu. Jumla ya Ng'ombe **9,278** walipigwa chapa na shilingi **12,846,050.00** zilitumika.

xii) Ukarabati wa josho katika kijiji cha Chiungutwa. Shilingi **385,550.00** zimetumika.

O. CHANGAMOTO ZA JUMLA

Pamoja na mafanikio tuliyoyapata mwaka huu, bado tuna changamoto kubwa zifuatazo:

i) Kuchelewa/Kutopokelewa kwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutoka Hazina. Mfano miradi ya CDG kiasi kilichopokelewa ni shilingi **400,000,000.00** kati ya shilingi **1,400,444,000.00** zilizobajetiwa.

ii) Uchakavu na upungufu wa miundombinu katika shule zetu za Msingi na Sekondari.

iii) Kukosekana kwa usafiri wa uhakika kwenye Halmashauri hivyo, kufanya ufuatiliaji wa miradi kukwama au kufanyika kwa kiasi kidogo, mfano Idara ya elimu Sekondari hakuna gari

iv) Upungufu wa Ofisi za kufanyia kazi uliopelekea kuwa na mazingira magumu ya kufanyia kazi.

v) Upungufu wa Watumishi kwa kada mbalimbali

P. UTATUZI WA CHANGAMOTO

i) Halmashauri kujipanga ili kukusanya zaidi kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ili kuweza kutekeleza miradi ya maendeleo kwa fedha za mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa fedha kutoka Serikali kuu.

ii) Fedha za Mfuko wa elimu ziende kutoa tija kwa sehemu zote zenye uhitaji zaidi na kuendelea kuihamasisha jamii kuchangia nguvu kazi katika miradi ya elimu.

iii) Halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari 1 katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2018/19.

iv) Halmashauri ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha jengo la Halmashauri ili Idara zote zilizopanga zipate ofisi na hivyo kupunguza gharama ya pango na changamoto zitokanazo na majengo hayo.
v) Halmashauri imepata kibali cha kuajili watumishi **54** katika bajeti ya mwaka 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii tena kukushukuru sana wewe na Baraza lako, Mhe. Mkuu wa Wilaya, Viongozi wa Chama, Wah. Wabunge, Wakuu wa Idara na Vitengo, Watumishi wote wa Halmashauri pamoja na wadau wote wa maendeleo kwa kujitoa kwenu katika kusimamia shughuli za maendeleo ndani ya Halmashauri yetu kwa mwaka 2017/18 na kuwaomba tushirikiane katika kutekeleza shughuli zote zilizopangwa katika mwaka mpya wa bajeti ya 2018/19 ili tuzidi kuiboresha Halmashauri yetu katika sekta zote ikiwemo Kilimo, Afya, Maji, Elimu na Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Changwa M. Mkwazu
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MASASI.